



KWA TOLEO LA MARA OJA

Mshirika wa Media: Renee Murphy
502.338.5377
(nambari ya simu)
Mark Hebert
502.322.4565
(nambari ya simu)

JCPS Kuhimiza Familia Kusashisha Habari za mawasiliano

Barua pepe ya sasa hivi na nambari za simu huhakikisha familia zinapata habari muhimu

Julai 29, 2020 – Shule za Umma za Kaunti ya Jefferson (JCPS) zinahimiza familia kuhakikisha ya kwamba habari zao za mawasiliano ni za kisasa, na zimesajiliwa kupokea ujumbe wa maandishi kutoka JCPS wakati wilaya inapojitayarisha kwa kuanzia kwa Mafunzo Yasiyo ya Kiasili (NTI).

Barua pepe za kisasa na nambari za simu zitakuwa muhimu kwa familia zinazohitaji kuomba Chromebook na/kidude kwa mwaka wa shule ujao. Mawasiliano kutoka kwa shule ya mwanafunzi na walimu pia yanahitaji barua pepe halali au nambari ya simu.

Pamoja na mabadiliko ya kazi na visa vya kufanyia kazi nyumbani, barua pepe zilizopo zinaweza kukosa kuwa halali. Kwa familia zizopokea barua pepe kutoka kwa wilaya na shule na ujumbe wa maandishi, hakuna hatua inayohitajika kwa wakati huu.

Ili kuhakikisha wazazi na walezi wanapokea habari kutoka kwa JCPS, wanahimizwa kuchukua hatua zifuatazo:

Ili kuhakikisha unapokea ujumbe wa maandishi, ingia tu kwa Mjumbe wa Shule kwa kutuma maandishi Y kwa 67587. **LAZIMA** uingie kwa mfumo huu ili kupokea ujumbe wa maandishi. Hata ikiwa JCPS wanayo namabri yako ya simu sahihi kwenye faili, hautaweza kupokea ujumbe wa maandishi ikiwa hujaingia kwenye Mjumbe wa Shule.

Ili kupokea barua pepe zako kutoka kwa wilaya na shule ya mtoto wako, lazima uwe na barua pepe yako ya kisasa katika mfumo wa JCPS. Habari inaweza kusasushwa katika Wavuti ya Mzazi. Ikiwa hauna kiingizi cha Wavuti ya Mzazi, unaweza kufungua akaunti hapa.

Ikiwa unayo akaunti iliyoko sasa, nenda kwa Wavuti ya Mzazi na ubonyeze “Ingia kwenye Wavuti ya Mzazi”

1. Chagua Mzazi wa Chuo
2. Weka hati ya kuingia (jina la mtumiaji na nywila)
 - a. Bonyeza Zaidi
 - b. Bonyeza Habari ya Familia
 - c. Bonyeza Sasisha (habari halisi na kasha bonyesha ‘Sasisha’ tena)

Familia ambazo awali “zilijiondoa” kutoka kwa barua pepe kutoka JCPS, au wakaripoti barua pepe kuwa barua taka, hawataweza kupokea barua pepe katika siku za usoni.

Siku ya kwanza ya JCPS imepengiwa kwa mnamo Agosti 25.

Fuata JCPS mtandaoni kwenye Facebook, Twitter, Instagram na YouTube.
JCPS